NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU
8 February 2013

Kwa Wabahai wa ulimwengu

Marafiki wapendwa,

*Katika jamii za kila ukubwa na uwezo,tunafurahi kuona michakato ya mpango wa miaka mitano ikiwasha mioyo ya huduma na kusisimua kitenda cha makusudi. Mifano inajitokeza kila siku ya jinsi gani kitendo cha kuiendea na kuigusa mioyo ya watu,kuijulisha mioyo hiyo neno la Mungu, na kuialika kuchangia kwenye uboreshaji wa jamii kinaweza, kwa wakati, kupelekea kwenye maendeleo ya watu. Mabadiliko haya ya pamoja huonekana wakati vidokezo vya mpango vinapojumuishwa katika juhudi za klasta zilizoenea na kuratibiwa vizuri, elimumiendo iendeleayo kujulikana. Klasta ya aina hiyo huwa kituo cha waumini wenye uzoefu kadri wale waliotambulishwa kwenye imani hivi karibuni, bila kujali umri au asili zao, kufanya kazi bega kwa bega, wakisindikizana katika huduma yao, kumuwezesha kila mmoja kushiriki katika utekelezaji wa mpango.*

*Kutoka katika mfululizo wa matukio katika ulimwengu wa kibahai uliojihusisha katika shughuli zenye ari, hususani jambo moja limetuvutia: mchango wa kimaamuzi uliotolewa na vijana katika kila bara. Katika jambo hili tunaona uthibitisho wa matumaini ya mpendwa mlinzi aliyoyawekeza kwao"kwa maendeleo ya baadaye na upanuzi wa hoja" na ya kujiamini ambayo aliweka mabegani kwao“ jukumu lote la utunzaji moyo wa huduma usiyo na ubinafsi miongoni mwa waumini wao". Tumevutiwa, pia, na idadi ya vijana ambao, baada ya ushirikiano wa muda mfupi na jamii ya kibahai, hujiwajibisha wenyewe kwenye vitendo vyenye maana vya huduma na kwa haraka hugundua mvuto wao kwenye juhudi za imani za ujengaji wa jamii. Kweli, katika kutafakari juu ya vijana wa kibahai na rika lao kimawazo, hatuwezi lakini kufurahia shauku yao kwenye kiwango cha majukumu kusaidia maendeleo ya kiroho na kijamii ya wale wawazunguukao, hususani wale vijana kuliko wao wenyewe. Katika kipindi kilichohaaribiwa na ubinafsi, ambamo hata ushirikishwaji wa kiroho unapimwa katika viwango vya zawadi na ridhaa binafsi, inatia moyo kuona watu binafsi kuanzia umri wa miaka 10 hadi miaka ishirini na kidogo — ambao juu yao mitazamo ya tamaa kali inafundishwa kwa makusudi — ambao wanaamshwa na mtazamo wa Baha'u'llah na wako tayari kuweka mahitaji ya wengine mbele kabla ya mahitaji ya wenyewe. Kwamba vijana hao wenye maadili, kwa kutumia juhudi zao wenyewe pamoja na mchepuko waisaidao jamii, lazima wawe wanachangia kwa nguvu kwenye juhudi kila mahali inaleta utabiri mzuri kwa ajili ya uchepushaji wa juhudi hizi.*

*Kile ambacho kimekuwa kikikamilishwa katika miaka miwili iliyopita kitakua, kwa hakika, kimevukwa mbali, si tu katika kuhitimisha miaka ya mpango huu wa sasa lakini miaka iliyosalia ya karne ya kwanza kipindi cha ujengaji. Kuhimiza juu ya jambo hili lenye nguvu na kuwakusanya vijana wa leo kuchukua majukumu kikamilifu ni lazima wajitokeze katika fursa hii muhimu, tunatangaza mwaliko wa mikutano 95 ya vijana, kati ya mwezi Julai na Oktoba, iliyopangwa mahali ambazo zinazunguka ulimwengu : Accra, Addis Ababa, Aguascalientes, Almaty, Antananarivo, Apia, Atlanta, Auckland, Baku, Bangalore, Bangui, Bardiya, Battambang, Bhopal, Bhubaneswar, Boston, Brasilia, Bridgetown, Bukavu, Cali, Canoas, Cartagena de Indias, Chennai, Chibombo, Chicago, Chisinau, Cochabamba, Daidanaw, Dakar, Dallas, Danane, Dar es Salaam, Dhaka, Dnipropetrovsk, Durham (United States), Frankfurt, Guwahati, Helsinki, Istanbul (2), Jakarta, Johannesburg, Kadugannawa, Kampala, Kananga, Karachi, Khujand, Kinshasa, Kolkata, Kuching, Lae, Lima, London, Lubumbashi, Lucknow, Macau, Madrid, Manila, Matunda Soy, Moscow, Mwinilunga, Mzuzu, Nadi, Nairobi, New Delhi, Oakland, Otavalo, Ouagadougou, Panchgani, Paris, Patna, Perth, Phoenix, Port-au-Prince, Port Dickson, Port Moresby, Port-Vila, San Diego, San Jose (Costa Rica), San Jose City (Philippines),*

*San Salvador, Santiago, Sapele, Sarh, Seberang Perai, South Tarawa, Sydney, Tbilisi, Thyolo, Tirana, Toronto, Ulaanbaatar,*
*Vancouver, Verona, Yaounde. Tunatoa mualiko kwenye mikusanyiko hii kwa kila kijana ambaye anatambua katika mbinu na zana za mikakati yenye nguvu ya mpango kwa ajili ya mchepuko kuelekea kwenye jamii bora. Na kwa kutoka kwa wabahai wa nyakati zote, tunakaribisha mchango wa dhati kwa washiriki ambao mambo mengi zaidi yanategemea juhudi zao.*

*Marafiki wapendwa: Kwa kila kizazi cha waumini vijana hujitokeza fursa ya kuchangia kwenye ustawi wa binadamu, ambayo ni ya kipekee katika kipindi cha uhai wao. Kwa kizazi cha sasa, wakati umefika kutafakari, kujihimu, kujiweka imara kwa ajili ya maisha ya huduma kutoka kwayo baraka zitamiminika kwa wingi. Katika sala zetu kwenye Kizingiti Kitakatifu, tunamsihi Uzuri wa Kale kwamba, kutoka katika jamii iliyovurugika na kukanganyika, Anaweza kutakaza roho safi na kujaliwa mtazamo wazi: vijana ambao uadilifu na unyoofu wao haukandamizwi kwa kujihusisha na makosa ya wengine na mabao hawazuiliwi na mapungufu yao wenyewe; vijana watakao mtazama Bwana na" kuleta wale waliotengwa katika duara la marafiki walioarifiwa"; vijana ambao utambuzi wao wa kasoro za jamii unawachochea kufanyia kazi mabadiliko yake, siyo kujitenga mbali nayo; vijana ambao, kwa gharama yoyote, watakataa kupitisha kwa dhuluma katika maumbo yake mengi na watatumia nguvu zao, badala yake, kwamba "mwanga wa haki utawanye wangavu wake juu ya ulimwengu mzima."*

*(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu)*

*Makao Makuu ya Wabahai ya Ulimwengu• S.L.P.155 • 3100101 Haifa, Israeli*
*Simu: 972 (4) 835 8358 • Nukushi: 972 (4) 835 8280 • Barua pepe: secretariat@bwc.org*